# MOTO JAMII TANZANIA

## MWONGOZO WA MAFUNZO KWA AJILI YA UELEWA NA ELIMU KUHUSU MOTO KATIKA NGAZI YA JAMII




United Republic of Tanzania

FIREWISE

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

**Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)**

Kwa kumbukumbu: TFS 2012. Mwongozo wa Mafunzo kwa ajili ya Uelewa na Elimu kuhusu Moto: Mafunzo katika ngazi ya kijiji, Tanzania. Dar es Salaam, ukurasa wa 71.

Design by DJPA; Printing by DeskTop Productions



## DIBAJI

Tanzania imekuwa ikitumia mbinu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu (Participatory Forest Management-PFM) tangu miaka ya 1990 kwa kupanua na kuboresha mikakati ya kuwashirikisha wadau ili kupata usimamizi endelevu wa misitu. Usimamizi wa Moto katika Ngazi ya Jamii ni moja ya mikakati ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ambao umeundwa kwa kushirikiana na wadau muhimu ili kuhakikisha Usimamizi Endelevu wa Misitu na usimamizi endelevu wa ardhi nchini. Kwa mantiki hii, ushiriki wa jamii katika usimamizi wa moto ni muhimu kwa mafanikio ya usimamizi wa maliasili katika jumuiya.

Katika miaka ya hivi karibuni, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (Tanzania Forest Services-TFS) imetambua kuwa mbinu pana na ya kina zaidi inahitajika ili kuhakikisha usimamizi endelevu wa ardhi nchini, kwa kuandaa mbinu za Usimamizi Jumuishi wa Moto (Integrated Fire Management - IFM) ili kuwa na usimamizi endelevu wa ardhi nchini. Mbinu za Usimamizi Jumuishi wa Moto ni pamoja na ukusanyaji taarifa, uzuiaji, maandalizi na uzimaji.

Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikiwezesha mafunzo mbalimbali juu ya usimamizi na uhifadhi wa misitu hasa juu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu na kuonyesha mafanikio katika hatua mbalimbali za mipango na utekelezaji. Licha ya uzoefu wa muda mrefu na mafanikio katika mbinu za Usimamizi Shirikishi wa Misitu nchini, masuala ya Usimamizi wa Moto wa Jamii (Community Based Fire Management -CBFiM) bado hayajaandaliwa na kutumika katika jumuiya zinazopakana na misitu.

Muundo na utekelezaji wa Usimamizi Jumuishi wa Moto katika ngazi ya jamii katika kutambua idadi ya matukio, ukali na usambaaji wa moto katika misitu na nyika Tanzania inamaana kwamba jamii hapa nchini zina umuhimu na ushawishi katika usimamizi wa moto. Umuhimu wa ushiriki wa jamii pia hushinikizwa na ukubwa wa nchi na kufikika kwa shida na miundombinu duni. Kwa hiyo, utekelezaji wa Usimamizi Jumuishi wa Moto nchini Tanzania ungeimarishwa zaidi kwa kuweka nia ya kuanzisha Usimamizi wa Moto wa Jamii na masuala yake mbalimbali katika utaratibu maalumu. Usimamizi wa Moto wa Jamii inatambua jukumu chanya na muhimu ambalo jumuiya zinaweza kusimamia katika usimamizi wa moto ikiwemo ufanyaji wa maamuzi kuhusu utumiaji na udhibiti wa moto.

Mwongozo huu wa "Jumuiya za MotoJamii" uliandaliwa ili kuzungumzia masuala ya msingi ya ushiriki wa jamii katika usimamizi wa moto. Uliandaliwa kwa kutumia mbinu shirikishi kwa ushirikiano na wadau wakuu kutoka sekta mbalimbali za usimamizi wa ardhi ikiwemo Idara ya Kilimo, Mifugo, Wanyamapori na nyinginezo kwa kuzingatia sheria na sera mbalimbali za nchi.

Kwa ujumla, mwongozo huu unazungumzia kipengele cha kwanza cha Usimamizi wa Moto katika Ngazi ya Jamii na unatia msisitizo katika:

a. Kujenga mwamko, ufahamu na maarifa kuhusu moto na matumizi ya moto ili kukuza kipato kinachotokana na maliasili;
b. Kuchangia mawazo juu ya uwezekano wa kuwa na kipato kisichotokana na matumizi ya moto kichaa;
c. Kuwezesha jamii kusimamia moto kwa manufaa yao na kupunguza athari hasi za moto; na
d. Kusaidia jamii katika kuanzisha, kuendeleza, kudhibiti na kutekeleza mwongozo wa moto wa kijiji, na kuzima moto usiotakiwa kwa kutumia mipango na programu shirikishi za kudhibiti moto katika jamii.

Uandaaji wa mwongozo huu wa mafunzo ulikuwa sehemu ya mradi wa usimamizi wa moto kwa

kushirikisha pande tatu katika nchi za Tanzania na Afrika ya Kusini uliofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani na kutekelezwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Mwongozo huu unawalenga wafanyakazi wa miradi ya sekta mbalimbali za usimamizi wa ardhi wanaoendesha mafunzo ya usimamizi shirikishi wa maliasili katika ngazi ya kijiji.

Juma S. Mgoo
Afisa Mtendaji Mkuu
Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

## SHUKRANI

Mwongozo huu umetayarishwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ulio chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Msaada wa kifedha kwa ajili ya maandalizi ya Mwongozo huu umetolewa na Serikali ya Ujerumani na ule wa kiufundi umetolewa na MotoJamii Afrika Kusini kupitia mradi wa Ushirikiano wa nchi tatu kwa ajili ya Usimamizi Jumuishi wa Moto (Integrated Fire Management -IFM) nchini Tanzania.

Shukrani za dhati zimwendee Anja Hoffmann (Mshauri kutoka GIZ) na Hein Krause (MotoJamii Afrika ya Kusini) kwa mchango na uvumilivu wao wakati wa maandalizi ya mwongozo huu. Shukrani nyingi ziende kwa Charles Ng'atigwa Mratibu wa Mradi wa TFS, kwa Felius Mwanalikungu (Sao Hill Forest Plantation) Feruzi Kiula (kanda ya Mashariki TFS), Theresia Massao (Kilombero Nature Reserve) pamoja na Taasisi ya Mafunzo ya Misitu (Forest Training Institute- FTI) iliyoko Olmotonyi kwa uhariri na upangiliaji wa mwongozo huu. Pia, shukrani ziwafikie washiriki wa programu ya mafunzo ya MotoJamii huko Olmotonyi wakiwemo wataalamu kutoka Idara ya Wanyamapori, Kilimo, Mifugo na Sekta nyingine. Michango yao katika mwongozo huu imekuza na kutanua dhana ya Usimamizi Jumuishi wa Moto Tanzania.
Tunawashukuru pia wanajamii wa vijiji vifuatavyo, Matanana, Mtili, Itimbo, Kitasengwa na Kihangwa vya wilaya ya Mufindi Mkoa wa Iringa na kwa kila mtu ambaye kwa njia moja au nyingine amechangia katika maandalizi ya mwongozo huu.

## VIFUPISHO

| | Kiswahili | English |
|---|---|---|
| UMJ | Usimamizi wa Moto wa Jamii | Community Based Fire Management (CBFiM) |
| TMM | Taasisi ya Mafunzo ya Misitu | Forestry Training institute (FTI) |
| SMKU | Shirika la Misaada ya Kimataifa la Ujerumani | Deutsche Gesellschaft fuer Internationale Zusammenarbeit (GIZ) |
| UJM | Usimamizi Jumuishi wa Moto | Integrated Fire Management (IFM) |
| UPM | Usimamizi wa Pamoja wa Misitu | Joint Forest Management (JFM) |
| USM | Usimamizi Shirikishi wa Misitu | Participatory Forest Management (PFM) |
| AK | Afrika ya Kusini | South Africa (SA) |
| WHM | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania | Tanzania Forest Service (TFS) |
| MUM | Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii | Fire Management Plan (FMP) |

## MISAMIATI NA MAANA ZAKE

| Madhara ya Moto | Athari hasi au chanya ya moto kwa mazingira |
|---|---|
| Udhibiti wa moto | Shughuli zote zinazohusiana na udhibiti na uzimaji wa moto kufuatia kugundulika kwake. (Neno jingine: Uzimaji Moto) Mbinu za uzimaji ni: Mashambulizi ya moja kwa moja - njia ambayo moto hushambuliwa mara moja karibu na mwako. Mashambulizi Sambamba - njia ambayo kinga-moto hujengwa jirani na moto ulipo kadri ambavyo joto na miale ya moto itakavyoruhusu, na kuchoma mwako katikati ya moto na kinga-moto. C Mashambulizi yasiyo ya moja kwa moja - njia ambayo mstari wa udhibiti moto huwekwa kimkakati ili kuitumia vizuri miundo asilia ya ardhi iliyo mbele zaidi ya mahali moto ulipo, na kinga-moto huchomwa moto au kulipuliwa. D) Uangaliaji wa Joto - njia ya kuangalia ueneaji na nguvu ya moto katika vile vituo ambavyo vinaonyesha usambaaji wa haraka au pengine vinavyoweza kuleta madhara katika udhibiti wa moto. Hii ni tofauti na utaratibu maalumu wa kufanya kazi maeneo yote ya moto kwa wakati moja, au katika hali mfululizo hatua moja baada ya nyingine. E) Ufuatiliaji wa baridi - njia ya kuangalia kama moto bado unawaka, inayohusisha ukaguzi makini na kushika kwa mikono, au kwa kutumia vipimo vya joto (infrared scanner) ili kugundua chanzo chochote cha joto. Uondoaji - kitendo cha kuzima moto uliobakia baada ya kuwa umedhibitiwa. |
| Maeneo Hatarishi ya Moto | Maeneo rahisi kushika moto |
| Usimamizi wa Moto | Shughuli za usimamizi wa moto zinajihusisha na ulinzi wa watu, mali, misitu na mapori kutokana na moto usiotakiwa. Pia inajihusisha na matumizi salama ya moto kama njia ya usimamizi wa ardhi. |
| Pembetatu ya Moto | Msaada wa kufundishia ambao unaonyesha pande za pembetatu zikiwakilisha vitu vitatu muhimu kwa ajili ya kuwasha na kuzalisha moto (yaani, oksijeni, joto na mwako). Wakati kimojawapo kati ya hivi vitu kitaondolewa, uzalishaji wa moto hauwezekani au utasitishwa. |
| Hali wa Hewa ya Moto | Hali ya hewa inayosaidia uwakaji wa moto, tabia na uzimaji wa moto |
| Mwako | Kitu chochote kinachoweza kuwaka moto ikiwemo mimea |
| Kamati ya Maliasili | Kamati iliyoundwa na baraza la kijiji na inayosimamiwa na Serikali ya Kijiji |
| Moto Uliokusudiwa au Unaosimamiwa | Moto wowote uliowashwa kutokana na maamuzi ya utawala ili kufikia malengo fulani ya usimamizi wa ardhi |
| Maeneo ya Usalama | Eneo linalotumika kujihifadhi wakati moto ukivuka Kinga-Moto, au wakati moto wa ghafla ukisababisha Mwako ulio nje ya Kinga-Moto kufanya eneo lililo ndani ya Kinga-Moto lisiwe salama tena |
| Wadau | Hawa ni watu na taasisi mbalimbali ambazo zinajishughulisha na shughuli mbalimbali za usimamizi wa moto |
| Moto Kichaa au usiosimamiwa | Moto ambao haukupangwa, na usiohitajika ikiwemo moto uliosababishwa na binadamu, matukio ya moto uliovuka kutoka katika uchomaji mapori, moto uliovuka kutoka katika miradi iliyopangwa na uchomaji mapori |
| Moto wa Nyika | Moto wowote usio na mpangilio ambao unatokea nyikani. Aina tatu za moto wa nyika zinazotambuliwa ni pamoja na moto usiodhibitika, matumizi ya moto katika mapori na moto ulioandaliwa kwa nia fulani |
| | |

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| **DIBAJI** | | **1** |
| **SHUKRANI** | | **3** |
| **VIFUPISHO** | | **4** |
| **MISAMIATI NA MAANA ZAKE** | | **4** |
| **HISTORIA YA MOTO TANZANIA** | | **6** |
| 1.1 | Dhana Ya Usimamizi Jumuishi Wa Moto Tanzania | 6 |
| 1.2 | Dhana Ya Motojamii Kama Sehemu Ya Usimamizi Wa Motojamii | 7 |
| **JINSI YA KUUTUMIA MWONGOZO HUU** | | **8** |
| 2.1 | Maandalizi Kwa Ajili Ya Mafunzo | 9 |
| 2.2 | Utunzaji Wa Kumbukumbu Za Mafunzo | 9 |
| 2.3 | Angalia Eneo La Mafunzo Kwa Ajili Ya Somo La Ukaguaji Wa Hatari | 10 |
| **3** | **VIPINDI VYA MAFUNZO KWA UFUPI** | **11** |
| 3.1 | Madhumuni Ya Mafunzo Na Ratiba | 11 |
| **4** | **UFUNGUZI: UTANGULIZI NA MALENGO** | **12** |
| 5 | Somo 1: Athari Chanya Na Athari Hasi Za Moto | 13 |
| 6 | Somo 2: Pembetatu ya Moto | 15 |
| 7 | Somo 3: Jamii Na Matumizi Ya Moto | 16 |
| 8 | Somo 4: Ushiriki Wa Jamii katika Usimamizi Wa Moto | 17 |
| 9 | Somo 5: Wajibu wa Jumuiya katika Usimamizi wa Moto | 19 |
| 10 | Somo 6: Uandaaji wa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii | 20 |
| 11 | Somo 7: Utambuaji wa Maeneo Hatarishi kwa Moto | 21 |
| **12** | **KIPINDI CHA KUTOA MREJESHO WA KILA SIKU** | **22** |
| **13** | **TATHMINI NA HITIMISHO** | **23** |
| 14 | Kiambatisho 1 | 24 |
| 15 | Kiambatisho 2 | 42 |
| 16 | Kiambatisho 3 | 46 |
| 17 | Kiambatisho 4 | 48 |
| 18 | Kiambatisho 5 | 50 |

# Historia ya Moto Tanzania

Moto umekuwa ukitumika Tanzania kwa miaka mingi katika kuandaa ardhi kwa ajili ya kilimo na malisho ya wanyama pamoja na shughuli za uwindaji, udhibiti wa wadudu waharibifu na kwa sababu nyinginezo za usimamizi wa ardhi. Moto unaowashwa na watu wa maeneo husika umechangia kutengeneza mfumo wa ikolojia na viumbe hai katika nyika ya Afrika na ikolojia ya misitu ya miombo. Moto ni nyenzo ya kufikia malengo ya usimamizi wa wanyamapori na uhifadhi. Kwa watu wa vijijini moto ni nyenzo muhimu kiuchumi katika kufikia madhumuni mbalimbali ya usimamizi wa ardhi. Mara nyingi jamii zina maarifa ya kijadi juu ya kusimamia na kuzuia moto. Hata hivyo, uwiano unaofaa kati ya watu, moto na mazingira ya asili umekuwa mgumu kufikiwa kutokana na mabadiliko ya idadi ya watu, vitendo vya usimamizi wa ardhi na vikwazo katika njia za usambazaji wa maarifa yanayotumika katika usimamizi wa maliasili. Kuna ongezeko la hofu juu ya hatma ya ongezeko la matukio ya moto na athari zake hasi katika misitu na maeneo ya mapori, pamoja na maisha ya binadamu katika hali iliyo na mabadiliko ya tabianchi.

Tafiti za hivi karibuni kutoka kwenye picha za satelaiti zimeonyesha kuwa wastani wa hekta milioni 11 huungua kila mwaka nchini Tanzania. Uchomaji mwingi hutokea katika mikoa ya magharibi ya nchi na nyanda za juu kusini hasa Rukwa, Tabora, Kigoma na Mbeya, wakati katika maeneo ya Kusini Mashariki, mkoa wa Lindi huathiriwa zaidi na moto. Aina ya ardhi inayoathiriwa zaidi ni mapori na ardhi yenye vichaka ambazo hufikia takribani asilimia 70 ya ardhi inayoungua kila mwaka yenye wastani wa hekta milioni 6.8 kwa mwaka. Uunguaji mwingi hutokea kwenye maeneo yaliyohifadhiwa, kwa wastani wa hekta milioni 3.7 kwa mwaka katika hifadhi za misitu, hekta milioni 3.3 katika hifadhi za wanyamapori na hekta milioni 1.46 katika mbuga za taifa, zikifikia jumla ya karibia hekta milioni 8.5 au asilimia 77 ya ardhi inayoungua kila mwaka nchini Tanzania.

## 1.1 Dhana ya Usimamizi jumuishi wa Moto Tanzania

Ingawa uchomaji wa mimea umekuwa ukihofiwa zaidi katika miaka ya hivi karibuni kutokana na athari zake za moja kwa moja katika mazingira na maisha ya binadamu, athari za moto hazijawa zenye athari mbaya peke yake, kwani si kila moto una madhara. Hivyo, kuendeleza mifumo ya ikolojia na usimamizi wa ardhi pamoja na malengo ya maisha kwa kupitia njia sahihi za usimamizi wa moto kunahitaji kutilia maanani athari zote za moto, zenye manufaa na zenye madhara. Dhana ya usimamizi jumuishi wa moto inatoa mfumo wa ujumla wa usimamizi wa moto katika ikolojia inayotegemea moto kama vile ikolojia ya nyika wakati pia ikizipa manufaa jamii zinazoizunguka pamoja na kuendeleza huduma za kiikolojia. Usimamizi Jumuishi wa Moto unahusisha vitu vitano ambavyo ni Kinga (kupunguza hatari), Kujiandaa (kuwa tayari), na Uzimaji (Uitikiaji), Urudishiaji (kwa kupitia ukarabati), ukusanyaji wa taarifa na uchambuzi (Utafiti). Vitu hivi vinahusisha vipengele pamoja na shughuli nyingine kwa kuzingatia mambo ya kimazingira, kijamii, kiuchumi na utawala wa kisiasa. Pia, jambo la muhimu ni kushirikisha wadau mbalimbali katika ushirikiano wa kitaasisi katika utekelezaji wa mipango muhimu ya kiufundi, kiutaratibu (lojistiki), kiutendaji na kijamii ili kuweka uwiano kati ya kuendeleza na kuhifadhi maliasili na kusimamia moto usiohitajika na wakati huo huo kuendeleza matumizi salama ya moto wenye manufaa.

## 1.2 Dhana ya MotoJamii kama sehemu ya Usimamizi wa Motojamii

Ndani ya mfumo unaoungwa mkono na GIZ wa mradi wa Ushirikiano wa Nchi Tatu ikiwemo Tanzania na Afrika ya Kusini kwa ajili ya Usimamizi Jumuishi wa Moto, msaada umekuwa ukitolewa kuwezesha Usimamizi Jumuishi wa Moto katika ngazi ya taifa na ngazi za chini Nchini Tanzania ili kupunguza makali ya athari zisizofaa za matukio ya moto usiohitajika ili wakati huo huo kuelimisha jamii zilizochaguliwa juu ya matumizi ya moto kama nyenzo ya usimamizi wa maliasili. Kutokana na mafunzo kutoka kwenye miradi ya "Kufanyia kazi Moto" (Working on Fire) na mradi wa MotoJamii iliyokuwa na mafanikio Afrika ya Kusini, shughuli mbalimbali na mbinu za mafunzo zinazofaa kukuza uelewa na kukuza mbinu za usimamizi wa moto zilibainishwa na kufanyiwa kazi. Kwa ujumla mradi ulitilia mkazo kwenye utambulishaji na utoaji wa mafunzo kuhusu dhana ya "MotoJamii" na kuandaa mtaala uliotolewa sehemu nyingine na kurekebishwa kukidhi hali za kiuchumi na kijamii na kiutamaduni kwa ajili ya kutumika vijijini Tanzania.

Dhana ya "MotoJamii" hapo awali ilianzishwa katika Amerika ya Kaskazini, ni njia ya usimamizi wa moto katika ngazi ya jamii inayofanya kazi ya kujenga ufahamu wa hatari ya moto nyikani na kufundisha wanajamii juu ya usimamizi na njia za kuzuia moto. Kipaumbele cha "MotoJamii" ni kulinda uhai, maisha na mazingira kabla ya moto kuanza na kusaidia jamii kuandaa mpango wa usimamizi wa MotoJamii iwapo kutatokea tukio la moto. Kipengele muhimu kwa dhana ya MotoJamii ni kwamba mpango huo ni wa kijamii na huendeshwa kulingana na jamii, kwa kutilia mkazo katika kuboresha ushirikiano na uratibu wa usimamizi wa moto. Ili kuwa na ufanisi, MotoJamii inahitaji mchakato shirikishi kutoka hatua ya kwanza. Mwaka 2006 mradi wa "Kufanyia kazi moto" wa Afrika ya Kusini ulianza kutumia mfano wa umoja wa nchi za Marekani.

Mradi wa ushirikiano wa nchi hizo tatu katika usimamizi wa moto ulianzisha MotoJamii Afrika ya Kusini (SA FireWise) kwa kufanya mafunzo kadhaa pamoja na kutathmini mfumo wa SA MotoJamii kwa ajili ya kutumika katika mazingira ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania ndani ya hatua zitakazohusisha washikadau kutoka kwa mawakala mbali mbali wa usimamizi wa ardhi. Mbali na utayarishaji huo wa mtaala, nyenzo saidizi za kimichoro ziliandaliwa ili kwenda sambamba na kusaidia wafanyakazi wa MotoJamii kushirikisha wanajamii juu ya masuala ya moto kwa njia ya majadiliano ya pamoja.a

# Jinsi ya Kuutumia Mwongozo Huu

Mwongozo huu uliundwa ili kuwapa uwezo wadau mbalimbali ambao wanahitaji kuwezesha mafunzo kuhusu moto katika jamii katika ngazi ya kijiji. Masomo mengi katika mwongozo huu yameandaliwa katika namna ya kuwawezesha washiriki kupata ujuzi na uelewa juu ya usimamizi wa moto katika ngazi ya jamii. Mwezeshaji ambaye anatumia mwongozo huu lazima awe na uelewa mzuri wa usimamizi wa moto katika ngazi ya jamii, pamoja na kuwa na uwezo wa kufundisha kwa kutumia mbinu shirikishi.

Mpangilio wa masomo mengi katika mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia kanuni za elimu ya watu wazima ili uzoefu wa washiriki wote uweze kuibua somo jipya. Masomo haya yana nguvu ya kujenga uwezo wa kamati mbalimbali za kijiji, mabaraza ya kijiji na makundi mengine kama yatatumika vizuri. Kwa maana hiyo, mwongozo huu unaweza kutumika katika hali tofauti kulingana na malengo, muda, aina ya washiriki na rasilimali zilizopo. Masomo ya mwongozo huu yameandaliwa kwa ajili ya kufanya mafunzo ya siku tatu ambayo yatajumuisha masuala muhimu katika kudhibiti moto katika misitu

Masomo katika mwongozo huu yamepangwa kwa mtiririko unaoleta maana. Hata hivyo, si lazima kufuata mtiririko huu kuanzia mwanzo hadi mwisho wakati wa mafunzo. Mwongozo huu umeundwa kuonyesha njia na umependekeza masomo yatakayogusia mada ambazo ziko katika mtiririko mzuri ili kukuongoza katika ufanyaji wa mazoezi na vitini mbalimbali kwa namna ipasayo. Unahimizwa kuutumia mwongozo kama ulivyo au kuubadili kama itakavyohitajika. Masomo yaliyoelezwa katika mwongozo huu yanabainisha mifano mbalimbali na pia kwa kutumia ubunifu wako, yatakusaidia kuandaa mafunzo bora.

Changamoto zinaweza kutokea wakati wa kutumia mwongozo huu. Kwa mfano, katika mchakato wa kutafsiri maneno ya Kiingereza kwenda kwenye Kiswahili, baadhi ya maneno yanaweza kupoteza maana yake, kwa hiyo ni muhimu kushirikisha wataalamu wenye uzoefu na usimamizi wa moto-jamii. Pia kuna baadhi ya mambo ambayo yanaweza kutumika kama yalivyo au yakabadilishwa ili kuendana na hali au mahali fulani kama vile mazoezi, chemsha bongo na mengineyo.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu kuu nne:

1. Sehemu ya kwanza inatoa maelekezo ya jinsi ya kutumia mwongozo huu,

2. Sehemu ya pili ina masomo kuhusu moto na jinsi ya kutumia na kudhibiti moto

3. Sehemu ya tatu inahusu maoni na tathmini

4. Sura ya nne ina viambatishi muhimu kama vile vitini vya washiriki na nyenzo nyingine kwa ajili ya mafunzo.

## 2.1 Maandalizi kwa Ajili ya Mafunzo

Ili kutumia mwongozo huu kwa ufanisi katika mazingira tofauti, ni muhimu kutilia maanani yafuatayo:

- Kuwa na malengo ya mafunzo yanayoeleweka.
- Mwezeshaji ambaye anatumia mwongozo huu ni lazima awe na malengo yanayoeleweka, ambayo yanawezekana kufikiwa; uelewekaji wa malengo utasaidia washiriki kuelewa mambo yanayotarajiwa kutoka kwao.
- Kuchangia mawazo bila ya kukanganyana
- Mwezeshaji lazima awahimize washiriki watumie mbinu za mafunzo zilizoainishwa katika mwongozo huu na pia kutoa fursa za majadiliano kuhusu mada husika. Jukumu la mwezeshaji ni kutoa changamoto kwa washiriki ambazo zitawafanya watake kujifunza zaidi.

### Mahali pa mafunzo

Ingawa mafunzo yanaweza kufanyika mahali popote, ni vizuri kuelewa mambo ya msingi ambayo yatasaidia kufikia mafunzo mazuri kwa wawezeshaji na washiriki. Jambo muhimu ni kuwa tayari kubadilika kulingana na mazingira. Kwa vile muda wote washiriki watakuwa wanahamahama ndani ya ukumbi, mwezeshaji anatakiwa apate mahali pa mafunzo penye utulivu na nafasi ya kutosha kuruhusu uhamishaji wa samani kama vile meza na viti. Vile vile, inawezekana kupanga viti chini ya kivuli cha mti kama haiwezekani kupata ukumbi wenye nafasi ya kutosha.

### Vifaa vya mafunzo na kitabu cha kumbukumbu

Kulingana na masomo yaliyoelezewa katika mwongozo huu, mwezeshaji atahitaji zana za mafunzo na kitabu cha kumbukumbu, chatipindu, kalamu ya wino usiofutika, kadi kufundishia na za vitambulisho vya majina, karatasi za ukubwa wa A4, mpira wa ufukweni, Gundi ya karatasi, madaftari ya kuandikia na penseli ili kufanikisha mchakato mzima wa mafunzo kwa washiriki.

## 2.2 Utunzaji wa Kumbukumbu za Mafunzo

### Uchukuaji wa kumbukumbu wakati wa mafunzo

Kama ambavyo shughuli za mafunzo huwa haziwi timilifu kabisa pindi mafunzo yanapofanyika kwa mara ya kwanza, mwezeshaji anahitaji kuendelea kuboresha mafunzo kadri yanavyoendelea. Njia bora ya kuboresha mafunzo ni kuandika na kuchukua taarifa ya mambo ambayo yanatokea. Mwezeshaji anaweza kufanya hivyo wakati wa mapumziko na nyakati za jioni au anaweza kumuomba mtu mwingine (mfano mwezeshaji mwenza) amsaidie kwenye kazi hii. Mara nyingi, mawazo mazuri huja wakati wa matukio, hivyo ni muhimu kuchukua taarifa haraka iwezekanavyo.

### Utunzaji wa kumbukumbu za matokeo

Mambo yote kuhusiana na chemsha bongo, uchangiaji mawazo, maoni ya kila siku na mazoezi mengine hujenga matokeo ambayo washiriki wangependa kuondoka nayo pindi wanaporudi makwao. Kuandika kwenye chatipindu huongeza usumbufu, lakini ni muhimu katika mafunzo.

Aina zote za utunzaji kumbukumbu huweza kufanyika kwa njia tofauti na watu tofauti. Ni muhimu kufikiria kuhusu nini, jinsi gani na nani atatunza kumbukumbu.

### Muda

Kabla ya kuendesha mafunzo, mwezeshaji anapaswa kuzingatia misimu ya mwaka. Hii itasaidia kuwapatia washiriki maeneo kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa urahisi, na pia ili wasikwamishe shughuli mbalimbali za kijamii. Pia, inapendekezwa kuendesha mafunzo kwa saa sita kwa siku ili kuwapa washiriki muda wa kufanya shughuli nyingine za jamii au shughuli binafsi.

## 2.3 Angalia eneo la Mafunzo kwa ajili ya somo la ukaguaji wa hatari

Ili kuweza kuendesha mafunzo kwenye somo la tathmini ya hatari, wakufunzi ni lazima wafike kabla ya muda wa mafunzo (kwa mfano, siku moja kabla ya kuanza mafunzo) katika eneo la mafunzo ili kubainisha mifano itakayotumika kwenye somo la ukaguaji wa hatari. Wakati wa somo, maeneo haya lazima yatembelewe na washiriki wa mafunzo na kujadiliwa kwa kuzingatia hatari ya moto na hatua za kuzuia moto. Maeneo haya yanaweza kuwa ni mashamba ya kilimo yaliyo jirani, maeneo ya uchomaji mkaa, mizinga ya nyuki na maeneo mengineyo.

# Vipindi Vya Mafunzo Kwa Ufupi

Kipengele hiki kinaelezea vipindi 10 vya mafunzo ambavyo vimepangwa katika moduli moja. Kila kipindi kinaenda sambamba na kitini kwa ajili ya washiriki (Kiambatisho 1) na michoro kwenye kadi za ukubwa wa A2.

## 3.1 Madhumuni ya Mafunzo na Ratiba

Mafunzo ya MotoJamii yanahusisha wadau mbalimbali ili kutambulisha mpango wa matumizi sahihi ya moto, usimamizi wa moto na uzimaji wa moto kwa kutumia njia sahihi katika jamii husika.

Madhumuni ya Mafunzo:

- Washiriki wataweza kuelezea maana ya usimamizi wa moto katika jamii
- Washiriki wataweza kuandaa na kutekeleza mipango ya usimamizi na udhibiti wa moto katika jamii

Kila siku wakati wa mchana, patakuwa na muda mfupi wa kuhitimisha mada ya mafunzo kwa siku hiyo na kipindi cha maoni.

Mafunzo yanatarajiwa kuchukua siku tatu kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:

| Muda | Siku 1 | Siku 2 | Siku 3 |
|---|---|---|---|
| Asubuhi | Kipindi cha ufunguzi: Utangulizi na malengo (saa 1 ½)<br>Somo 1: Athari chanya na athari hasi za moto (Saa 2) | 1. Mapitio ya Siku 1 (Maswali na Majibu, Saa ½)<br>2. Somo 3: Jamii na matumizi ya moto (Saa 2)<br>3. Somo 4: Ushiriki wa Jamii katika usimamizi wa moto (Saa 2) | 1. Mapitio ya Siku 2 (Maswali na majibu, Saa ½ )<br>2. Somo 6: Kuandaa mpango wa usimamizi wa moto (Saa 2 ½ )<br>3. Somo 7: kubainisha maeneo hatarishi ya moto (zoezi la nje hadi masaa mawili) |
| Mchana | Somo 2: Pembetatu ya Moto (Saa 2)<br>Kufunga siku na kutoa maoni (Saa 1) | 4. Somo 5: Majukumu ya Jamii katika Usimamizi wa Moto (Saa 2)<br>5. Kufunga Siku 2 na kutoa maoni ( ½ saa) | 4. Somo 7 linaendelea na mazoezi katika maeneo ya mafunzo na kumalizia uandaaji wa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii<br>5. Tathmini na hitimisho |

Kipindi kifupi kwa ajili ya maoni kitafanyika kila mwisho wa siku, na katika siku ya mwisho ya mafunzo tathmini ya mwisho ya mafunzo itafanyika.

# Ufunguzi: Utangulizi na Malengo

| Ufunguzi: Utambulisho wa washiriki na utambulisho wa yaliyomo kwenye mafunzo | |
|---|---|
| MALENGO | Baada ya kipindi hiki washiriki wataweza kufanya yafuatayo:-<br>1. Kujua mipangilio yote ya kiutawala na kitaratibu (lojistiki)<br>2. Kufahamiana baina ya washiriki na wakufunzi<br>3. Kuelewa malengo ya mafunzo ambayo ni kujenga uelewa na ujuzi kwenye jumuiya juu ya moto-kichaa (moto usiodhibitika) ili kupunguza athari za moto huo na kusisitiza matumizi sahihi ya moto.<br>4. Kukubaliana katika kanuni na hatua za mafunzo |
| NYENZO | • Kujua mipangilio yote ya kiutawala na kitaratibu (lojistiki)<br>• Kufahamiana baina ya washiriki na wakufunzi<br>• Kuelewa malengo ya mafunzo ambayo ni kujenga uelewa na ujuzi kwenye jumuiya juu ya moto-kichaa (moto usiodhibitika) ili kupunguza athari za moto huo na kusisitiza matumizi sahihi ya moto.<br>• Kukubaliana katika kanuni na hatua za mafunzo |
| MUDA | Saa 1 ½ |
| HATUA | 1. Kiongozi wa eneo husika anatakiwa kumkaribisha Mwezeshaji mkuu ajitambulishe mwenyewe na jopo la wawezeshaji<br>2. Mwezeshaji awaombe washiriki wajitambulishe kwa kutaja majina yao, nyadhifa na shughuli wanazofanya.<br>3. Kila mshiriki anapaswa kuandika jina lake na kuliweka mbele ya meza yake au avae kifuani.<br>4. Mwezeshaji afafanue malengo na ratiba ya mafunzo kwa kutumia chatipindu<br>5. Mwezeshaji atoe vifaa vya mafunzo kwa washiriki kama vile madaftari, kalamu, vitini na mada ya mafunzo.<br>6. Mwezeshaji awaongoze washiriki kuandaa sheria ambazo zitatumika wakati wa mafunzo.<br>7. Mwezeshaji aandike sheria ambazo wamekubaliana katika karatasi ya kufundishia.<br>8. Mwezeshaji awaombe baadhi ya washiriki wa kujitolea kuunda timu mbili, ambazo ni timu za huduma na timu za viburudisho ambazo zitafanya kazi kwa kubadilishana.<br>9. Mwezeshaji anapaswa kubainisha majukumu ya kila timu.<br>10. Mwezeshaji aelezee kwa ufupi jinsi mafunzo yatakavyofanyika.<br>11. Mwezeshaji aelezee kwamba katika mafunzo haya, washiriki watapata fursa ya kuchangia kwa kutoa maoni yao, mapendekezo na uzoefu wao ili maarifa yatakayopatikana kutoka kwenye mafunzo haya yaweze kutumika katika maeneo yao.<br>12. Katika mafunzo haya, kila somo linahusiana na somo lililopita na somo litakalofuatia. Hivyo inashauriwa kwamba washiriki wahudhurie vipindi vyote bila kukosa ili waweze kupata mtiririko mzuri wa mafunzo<br>13. Mwezeshaji afunge kipindi kwa kuwahimiza washiriki kutoa maoni yao kwa kadri wanavyoweza |
| MAONI | 1. Washiriki waliochelewa wapewe nafasi ya kujitambulisha<br>2. Kanuni ambazo zinaweza kuwekwa ni pamoja na: -<br>• Zima mlio wa simu yako au weka kwenye mzizimo<br>• Wazo la kila mshiriki linapaswa kuheshimiwa.<br>• Washiriki lazima wazingatie muda.<br>• Kila mshiriki anatakiwa kushiriki kikamilifu<br>3. Mchunga muda achaguliwe kutoka kwenye timu ya huduma<br>4. Kuwepo na maoni juu ya somo lililopita baada ya kila siku mpya ya mafunzo |

# Athari Chanya Na Athari Hasi Za Moto

| Somo 1: Athari Chanya na Hasi za Moto | |
|---|---|
| MALENGO | Somo hili lidhihirishe maarifa ya washiriki kuhusu moto na athari ya moto katika mazingira yao. Ni lazima pia ligusie maarifa ya ndani na ya kijadi, jinsi moto unavyoweza kutumiwa vyema na wapi moto huwa ni tishio kwao. Mwishoni mwa kipindi, washiriki wataweza kuelewa athari hasi na chanya za moto. |
| NYENZO | • Chatipindu<br>• Kalamu ya wino usiofutika<br>• Gundi ya karatasi<br>• Kadi Maalum za kufundishia<br>• Kitini: Athari za moto |
| MUDA | Saa 2 |
| HATUA | 1. Mwezeshaji aanze kipindi kwa kuelezea kwamba, wakati wa somo hili watajadili athari chanya na athari hasi za moto katika mazingira yao ya vijijini.<br>2. Mwezeshaji awaulize washiriki kuhusu uzoefu wao juu ya athari chanya na athari hasi za moto zinazoathiri maisha yetu na mazingira.<br>3. Mwezeshaji awagawe washiriki katika vikundi vinne vyenye washiriki watano au zaidi katika kila kundi kwa utaratibu wa kuhesabu namba 1-5, wale ambao watahesabiwa namba moja watajenga kundi la kwanza, namba mbili watakuwa kundi la pili vivyo hivyo kwa namba tatu, nne na tano.<br>4. Makundi yote yatatumia muda wa dakika 30 kwa ajili ya majadiliano na waandike kwenye chatipindu angalau athari chanya tatu na athari hasi tatu za moto.<br>5. Mwishoni, mwezeshaji akiambie kila kikundi kichague mwakilishi mmoja atakayewasilisha athari za moto zilizojadiliwa katika kikundi. Baada ya kundi la kwanza, mwezeshaji atakaribisha kundi la pili kuwasilisha bila kurudia yale yaliyokuwa yametolewa na washiriki wenzao,<br>6. Baada ya kila kikundi kuwasilisha kazi zao, mwezeshaji aongeze athari nyingine ambazo hazijatajwa na kutoa maoni yake (kwa mfano athari ya moto kwenye mzunguko wa maji kama msitu utatoweka). Atafunga kipindi kwa kueleza jinsi madhara ya moto yanahusiana na maisha yetu ya kila siku na kusema kwamba ni lazima tusimamie moto ili kupunguza madhara yake hasi. |
| MAONI | |

| | |
|---|---|
| NYENZO ZINAZOTUMIKA |  |
| NYENZO ZINAZOTUMIKA | Bora, upunguzaji wa Mwako, uchomaji wa maeneo mbalimbali. |

# Pembetatu ya Moto

| Somo 2: Pembetatu ya Moto | |
|---|---|
| MALENGO | Mwishoni mwa kipindi hiki washiriki wataweza kuelezea pembetatu ya moto |
| NYENZO | • Kalamu ya wino usiofutika<br>• Chatipindu<br>• Gundi ya karatasi<br>• Kitini: Pembetatu ya Moto |
| MUDA | Saa 2 |
| HATUA | 1. Mwezeshaji awakumbushe washiriki kwa ufupi kuhusu waliyojifunza katika somo lililopita<br>2. Mwezeshaji aelezee malengo ya somo hili.<br>3. Mwezeshaji awaambie washiriki watoe mifano mitatu inayoelezea pembetatu ya moto<br>4. Mwezeshaji awasaidie washiriki wajigawe wenyewe katika makundi matatu (3).<br>5. Mwezeshaji awaeleze washiriki vitu vitatu vya pembetatu ya moto (vinavyohitajika kuanzisha na kufanya moto uendelee kuwaka kama vile joto, oksijeni na Mwako)<br>6. Mwezeshaji awaombe washiriki wajadili jaribio la kuzuia moto kwa kutumia pembetatu moto<br>7. Mwezeshaji alisaidie kundi la kwanza (1) kujadili jaribio la kuondoa oksijeni, kundi la pili (2) kujadili jaribio la kuondoa joto na kundi la tatu (3) kujadili jaribio la kuondoa Mwako. Mwezeshaji atoe dakika 15 kwa ajili ya majadiliano.<br>8. Mwezeshaji aombe mtu mmoja ajitolee kutoka kila kikundi na kuelezea majaribio waliyojadili na kuandika mambo muhimu ya kuzingatiwa kwenye chatipindu wakati wa zoezi hilo.<br>9. Mwezeshaji ahimize washiriki wazingatie mambo ya muhimu zaidi wakati wa usimamizi wa moto.<br>10. Mwezeshaji afunge somo kwa kugawa vitini kwa washiriki |
| NYENZO ZINAZOTUMIKA |  |

# Jamii Na Matumizi Ya Moto

| Somo 3: Jamii Na Matumizi Ya Moto | |
|---|---|
| MALENGO | Ifikapo mwisho wa somo hili, washiriki watakuwa wamepitia jinsi gani wanatumia moto katika maisha yao ya kila siku, jinsi walivyoweza kusimamia moto kijadi katika siku za nyuma na jinsi ya kusimamia moto wakati uliopo. Watajifunza kuhusu matumizi salama ya moto kwa ajili ya kuendeleza maisha na kuhifadhi mazingira. |
| NYENZO | • Chatipindu (andaa maswali kutokana na matumizi ya moto)<br>• Kalamu ya wino usiofutika<br>• Gundi ya karatasi<br>• Kitini |
| MUDA | Saa 3 |
| HATUA | 1. Mwezeshaji aelezee litakalojadiliwa<br>2. Mwezeshaji awaombe washiriki wajipange katika miduara miwili yenye idadi sawa ya washiriki (Mduara mmoja uwe ndani ya mduara mwingine). Miduara iandaliwe kwa namna ambayo kila mshiriki katika mduara mmoja atakuwa anaangaliana na mshiriki katika mduara mwingine<br>3. Mwezeshaji aulize maswali ambayo yatajadiliwa na washiriki wawili wanaotazamana<br>a. Ni kwa sababu zipi moto hutumika kwenye jamii?<br>b. Wanajamii wanatumiaje moto?<br>c. Wanajamii wanaudhibiti vipi moto?<br>d. Kuna njia za kijadi ambazo moto hutumika?<br>4. Baada ya dakika 5 mduara wa nje usogee hatua tatu kulia na kujadili swali jipya na mshiriki mwingine<br>5. Baada ya dakika 5 mduara wa ndani usogee hatua 5 kulia na kujadili swali jingine kwa namna ile ile<br>6. Mwezeshaji awapitie washiriki kuona majadiliano yao yanaendaje |
| MAONI | Njia ya majadiliano inapaswa kutumika kwa makini kwa sababu wakati mwingine huingilia mfumo wa kijadi (Ni vigumu kwa baba au mama mkwe kuangaliana uso kwa uso na wakwe zao)<br>Wakati wa majadiliano, washiriki wanapaswa kujadiliana kwa sauti ili mwezeshaji aweze kusikia na kufuatilia majadiliano<br>Kama washiriki ni wachache mwezeshaji anaweza kutumia mfumo mwingine ambao anadhani unafaa zaidi. |
| NYENZO ZINAZOTUMIKA |  |

# Ushiriki Wa Jamii katika Usimamizi Wa Moto

| Somo 4: Ushiriki wa Jamii Katika Usimamizi wa Moto | |
|---|---|
| MALENGO | Ifikapo mwisho wa kipindi kila mshiriki ataweza kuelezea nani ni mwanajamii na maana ya ushirikishwaji katika usimamizi wa moto kwa mtazamo wake |
| NYENZO | • Chatipindu<br>• Kalamu ya wino usiofutika,<br>• Gundi ya karatasi<br>• Kadi maalum ya kufundishia<br>• Kitini: Ushiriki wa Jumuiya katika Usimamizi wa moto |
| MUDA | Saa 2 |
| HATUA | 1. Mwezeshaji awaelezee washiriki kuwa kabla ya kujadili kwa kina juu ya ushiriki wa jamii katika usimamizi wa moto, tutajadili kwa kina maana ya jamii (kwa mfano nani ni mwanajamii) na majukumu yao katika maisha ya kila siku ya jumuiya.<br>2. Mwezeshaji awaambie washiriki kuwa "jamii" na "ushiriki" ni vitu vinavyotegemeana katika usimamizi wa moto.<br>3. Mwezeshaji awaombe washiriki wajigawe wenyewe katika makundi manne kwa kuhesabu namba 1 hadi 4. Ambao watataja namba 1 watakuwa katika kundi moja na kadhalika.<br>4. Mwezeshaji aelezee majukumu ya kila kundi:<br>a. Kundi la 1 & 3 watajadili faida za jamii kujishirikisha katika usimamizi wa moto.<br>b. Kundi 2 & 4 watafanyia kazi namna ya kushirikisha jamii katika usimamizi wa moto (kwa kutaja kamati zinazopatikana katika kijiji chao na kubainisha kamati ambayo inafaa kushughulikia usimamizi wa moto, kamati hizo lazima ziwe ziliundwa kulingana na mfumo uliopo wa serikali)<br>c. Mwezeshaji atoe dakika 45 kwa ajili ya majadiliano na kuwaambia washiriki waandike kila swali kwenye kadi zao maalumu za kufundishia za mipango.<br>5. Katika mwisho wa muda uliotolewa, mwezeshaji aliambie kila kundi liwasilishe kazi ya kikundi kwa darasa zima,<br>6. Wanapaswa kuanza na kundi 1 na 3, na kufuatiwa na majadiliano na ushauri kutoka kwa makundi mengine na kisha watatakiwa na kukubaliana juu ya mapendekezo yaliyotajwa kuhusu faida za ushiriki wa jamii kwenye usimamizi wa moto.<br>7. Kundi la 2 na 4 litafuata mfumo wa kundi la 1 na 3. Mwezeshaji anaweza kuongezea yale ambayo washiriki watasahau kuorodhesha kuhusu faida za ushiriki wa jumuiya na jinsi jumuiya zinavyoweza kushiriki katika usimamiaji wa moto.<br>8. Kadi maalum za kufundishia zote za mipango zibandikwe kwenye chatipindu<br>9. Mwezeshaji aelezee kwa ufupi yale yaliyowasilishwa na makundi<br>10. Mwezeshaji agawe vitini vyenye mifano inayoonyesha ushiriki wa jamii katika usimamizi wa moto<br>11. Mwezeshaji afunge somo kwa kuelezea kwamba watu tofauti wanaweza kuwa na mitazamo tofauti juu ya manufaa ya usimamizi wa moto. Ukihitaji kuudhibiti moto, jamii lazima iwe imeandaliwa vyema kama ambavyo itajadiliwa katika somo linalofuata. |

| | |
|---|---|
| NYENZO ZINAZOTUMIKA |   |

# Wajibu wa Jumuiya katika Usimamizi wa Moto

| Somo 5: Wajibu Wa Jumuiya katika Usimamizi Wa Moto | |
|---|---|
| MALENGO | Ifikapo mwisho wa kipindi, washiriki wataweza kuelewa majukumu ya jamii katika usimamizi wa moto |
| NYENZO | • Chatipindu<br>• Kalamu ya wino usiofutika<br>• Gundi ya karatasi<br>• Kitini: Wajibu wa jamii kwenye usimamizi wa moto |
| MUDA | Saa 2 |
| HATUA | 1. Mwezeshaji awaambie washiriki wajikumbushe kwa kutaja faida na jinsi ya kushirikisha jamii katika usimamizi wa moto kama ilivyojadiliwa katika somo lililopita kwa kuwaambia mmoja baada ya mwingine wataje faida na jinsi ya kushirikisha jamii katika usimamizi wa moto bila kujali mtiririko wa kutaja vitu hivyo.<br>2. Mwezeshaji aelezee kwamba kama tunahitaji kulinda misitu yetu na mali, basi inatupasa kujiandaa wenyewe kudhibiti matishio ya moto.<br>3. Mwezeshaji awaambie washiriki kubainisha majukumu mbalimbali ya jamii katika maeneo yao ya usimamizi wa moto.<br>4. Mwezeshaji awakaribishe washiriki ili wabainishe vitu wanavyoweza kufanya ili kupambana na moto usiohitajika kwa kuwagawanya katika makundi madogo kutokana na idadi ya kazi kama zilivyoainishwa katika hatua namba 3.<br>5. Kila kundi kibainishe namna watakavyokamilisha kazi waliyopewa<br>6. Baada ya dakika 10, mwezeshaji ayaambie makundi yajadili kwa pamoja majukumu ya jamii katika usimamizi wa moto.<br>7. Mwezeshaji anakili mawazo kutoka kila kikundi kwenye chatipindu. Anaweza kuuliza maswali kama kuna haja ya kufanya hivyo.<br>8. Baada ya makundi yote kushiriki katika kujadili matokeo, mwezeshaji aelezee kwa ufupi na kuwauliza washiriki kama wanakubaliana na walichosema kuwa watafanya katika kudhibiti moto.<br>9. Mwezeshaji ahitimishe kwa kuwahimiza washiriki kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza majukumu yaliyotajwa hapo juu. Kisha awaeleze washiriki kuhusu mustakabali wa jumuiya na matumizi sahihi ya moto. |
| NYENZO ZINAZOTUMIKA |  |

# Uandaaji wa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii

| Somo 6: Uandaaji wa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii | |
|---|---|
| MALENGO | Mpaka sasa washiriki wamejifunza na kujadili juu ya faida na hasara za moto, jinsi wanavyotumia moto katika maisha ya kila siku, jinsi watakavyotumia moto kwa usalama, jinsi ya uanzishaji wa kamati za vijiji zitakazoshughulikia usimamizi wa moto. Kwa sasa wanaweza kufikiria njia ya kuandaa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii kwa ajili ya vijiji vyao au eneo la jumuiya kwa kubainisha maeneo hatari na njia za pamoja za kuzuia na kuzima moto. |
| NYENZO | • Chatipindu.<br>• Kalamu ya wino usiofutika.<br>• Gundi ya karatasi.<br>• Kitini: Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii. |
| MUDA | Saa 2 |
| HATUA | 1. Mwezeshaji awaelezee washiriki faida za kuwa na Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii (MUM) kwa kuwashirikisha washiriki kujadili juu ya somo liliopita na jinsi gani wanaweza kutumia maarifa hayo kuunda shughuli zinazohusiana na moto katika mpango wa usimamizi.<br>2. Mwezeshaji awaeleze maana ya Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii:<br>3. Iwapo maswali yatajitokeza kutoka kwa washiriki, mwezeshaji atoe maelezo zaidi/majibu<br>4. Mwezeshaji awaambie washiriki watengeneze makundi kwa kuhesabu namba 1 mpaka 3. Washiriki watakaotaja namba 1 wataunda kundi namba 1 na kadhaliaka<br>5. Mwezeshaji atakipa kila kikundi chatipindu na Kalamu ya wino usiofutika<br>6. Kila kundi lijadili kwa kina kwa dakika 10 na kuandika mawazo yao kwenye chatipindu, "Nani ana wajibu wa kuandaa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii, mambo ya kuzingatia katika kujenga ufahamu wa jamii kuhusu usimamizi wa moto"<br>7. Mwezeshaji aombe mtu mmoja kutoka kila kundi ajitolee kuwasilisha yaliyojadiliwa na kundi lake<br>8. Mwezeshaji aruhusu majadiliano na maelezo zaidi kutoka kwa yaliyowasilishwa na vikundi<br>9. Mwezeshaji aelezee muundo wa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii na atoe hitimisho kwa kugawa vitini kwa washiriki |
| MAONI | Mwezeshaji awe na ufahamu wa kutosha kuhusu Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii. |
| NYENZO ZINAZOTUMIKA |  |

# Utambuaji wa Maeneo Hatarishi kwa Moto

<table>
<tr><th colspan="2">Somo 7: Utambuaji wa maeneo hatarishi kwa moto</th></tr>
<tr><td>MALENGO</td><td>Kuainisha maeneo hatarishi kwa moto katika eneo la kijiji ni sehemu ya Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii. Mwishoni mwa somo, washiriki wataweza:<br>1. Kutofautisha kati ya maeneo yaliyo salama na maeneo hatarishi kwa moto .<br>2. Kutathmini maeneo hatarishi kwa moto</td></tr>
<tr><td>NYENZO</td><td>• Chatipindu.<br>• Kalamu ya wino usiofutika.<br>• Gundi ya karatasi.<br>• Kitini: Utambuaji wa maeneo  hatarishi kwa moto.</td></tr>
<tr><td>MUDA</td><td>Mpaka saa 3</td></tr>
<tr><td>HATUA</td><td>1. Mwezeshaji awashirikishe washiriki kuchambua vyanzo vya moto<br>2. Mwezeshaji aeleze kuwa kwenda kinyume na mipango miji kutafanya eneo liwe kwenye hatari ya moto<br>3. Mwezeshaji aeleze maana ya maeneo hatarishi kwa moto  na jinsi ya kuyabadili yasiwe kwenye hatari ya moto<br>4. Iwapo maswali yatajitokeza kutoka kwa washiriki, mwezeshaji atoe maelezo zaidi au majibu<br>5. Mwezeshaji awaambie washiriki watengeneze makundi kwa kuhesabu namba 1 mpaka 3. Washiriki watakaotaja namba 1 wataunda kundi namba 1 na kadhaliaka<br>6. Mwezeshaji akipe kila kikundi chatipindu na Kalamu ya wino usiofutika<br>7. Kila kundi lijadili kwa kina kwa dakika 20 na kuandika mawazo yao kwenye chatipindu, "namna ya kutambua maeneo hatarishi kwa moto na uhamasishaji wa usimamizi wa moto"<br>8. Mwezeshaji atayarishe jedwali kama inavyoonyeshwa chini na kuibandika kwenye chatipindu</td></tr>
</table>

| Vyanzo vya maeneo hatarishi kwa moto | Njia za kurekebisha |
|---|---|
| | |
| | |

| | |
|---|---|
| HATUA | 9. Mwezeshaji aombe mtu mmoja kutoka kwenye kila kikundi ajitolee kuwasilisha yaliyojadiliwa na kikundi chake<br>10. Mwezeshaji aruhusu majadiliano na maelezo zaidi kutoka kwenye yaliyowasilishwa na vikundi<br>11. Baada ya hitimisho la somo la kwanza, mwezeshaji aelezee namna ya kufanya tathmini ya maeneo hatarishi kwa moto<br>12. Mwezeshaji agawe vitini kwa washiriki na aelezee vitu muhimu ambavyo viko kwenye vitini hivyo kwa kulinganisha na yaliyojadiliwa<br>13. Mwezeshaji ahitimishe somo kwa kuwahimiza washiriki kupunguza vyanzo vya maeneo hatarishi kwa moto |
| MAONI | Mwezeshaji awe na ufahamu wa kutosha kuhusu njia za kupunguza maeneo hatarishi kwa moto |

# Kipindi Cha Kutoa Mrejesho Wa Kila Siku

<table>
<tr><th colspan="2">Somo 8: Maoni</th></tr>
<tr><td>MALENGO</td><td>Kipindi cha maoni lazima kifanyika kila mwisho wa siku. Kinaweza kuwa kifupi lakini kitasaidia kuelewa:<br>1. Uelewa wa washiriki juu ya mada iliyowasilishwa.<br>2. Jinsi gani washiriki wameelewa mada ya siku</td></tr>
<tr><td>NYENZO</td><td>• Chatipindu iliyoandikwa "Tulichojifunza"<br>• Kalamu ya wino usiofutika<br>• Gundi ya karatasi<br>• Kadi maalum ya kufundishia<br>• Michoro kwenye chatipindu inayoonyesha hali za "furaha, kawaida na huzuni"</td></tr>
<tr><td>MUDA</td><td>Dakika 30</td></tr>
<tr><td>HATUA</td><td>1. Mwezeshaji atoe utangulizi wa mada,<br>2. Mwezeshaji aandae chatipindu iliyogawanywa katika sehemu tatu zilizochorwa nyuso tofauti (furaha, kawaida na ya huzuni)<br>3. Mwezeshaji atoe muhtasari wa yale waliyojifunza.<br>4. Mwezeshaji awaulize washiriki jinsi wanavyojisikia kuhusu siku hiyo. Kila mshiriki aandike sababu kwenye kadi na kuiweka chini ya uso ambao unawakilisha hali anayojisikia siku hiyo<br>5. Mwezeshaji awaambie washiriki waandike angalau jambo moja ambalo amejifunza kwenye kadi ya pili na kuiweka kwenye chatipindu iliyoandikwa "tulichojifunza"<br>6. Mwezeshaji asome kadi zilizowekwa kwenye chatipindu yenye kuonyesha hisia za washiriki na mambo waliyojifunza na kutunza kumbukumbu kwa ajili ya kuziwasilisha kwa washiriki siku inayofuatia.<br>7. Mwezeshaji atoe matokeo siku inayofuatia</td></tr>
</table>

| J | K | L |
|---|---|---|
| Furaha | Kawaida | Huzuni |
| Kwa nini | | |

# Tathmini Na Hitimisho

<table>
<tr><th colspan="2">Tathmini Na Hitimisho</th></tr>
<tr><td>MALENGO</td><td>Ifikapo mwisho wa mafunzo, mwezeshaji atakuwa anaweza: -<br>1. Kujua iwapo washiriki wameelewa mada husika wakati wa mafunzo.<br>2. Kupata maoni ya washiriki ambayo yatasaidia kuboresha mafunzo ya aina hiyo.</td></tr>
<tr><td>NYENZO</td><td>• Chatipindu<br>• Maswali manne yaliyoandikwa kwenye chatipindu</td></tr>
<tr><td>MUDA</td><td>Saa 1</td></tr>
<tr><td>HATUA</td><td>1. Mwezeshaji atambulishe lengo la kufanya tathmini kwa kutumia "Bakuli ya Samaki"<br>2. Mwezeshaji aeleze jinsi njia ya "Bakuli ya Samaki" itakayotumika<br>3. Mwezeshaji awaombe washiriki wasimame na kupanga viti vyao kwenye miduara (wa ndani na wa nje), idadi ya viti vya mduara wa ndani iwe ni ¼ ya washiriki na kiti kimoja cha ziada<br>4. Mwezeshaji atawaambia ¼ ya washiriki wakae kwenye mzunguko wa ndani kuwakilisha samaki. Kiti kimoja kibaki wazi ambapo ¾ ya washiriki watakaa kwenye viti vya mzunguko wa nje wakiwakilisha binadamu.<br>5. Mwezeshaji awaambie washiriki kwamba wakati zoezi hili likiendelea samaki wanaweza kuongea kwa sauti wakati binadamu hawaruhusiwi kuongea, bali wasikilize kwa makini.<br>6. Mwezeshaji atauliza swali la kwanza na atawahitaji samaki walijadili kwa umakini. Mtu yoyote kutoka kwenye viti vya mduara wa nje anayehitaji kuchangia mawazo yake itambidi akae kwenye kiti cha ziada na kuwa samaki, baada ya kuchangia mawazo yake atainuka na kukiacha kiti wazi.<br>7. Mwezeshaji atawaambia samaki wajadiliane kwa dakika 10 na kujibu maswali yatakayoulizwa<br>8. Wakati samaki wanajadiliana, mwezeshaji ataandika vitu muhimu kutoka kwenye majadiliano hayo kwenye chatipindu ili watu wote waone<br>9. Baada ya dakika 10 mwezeshaji atawakaribisha binadamu wajitolee kuwa samaki wapya na kurudia mlolongo kuanzia hatua ya 5-8 wakati wakijadiliana swali la pili mpaka maswali yote manne yatakapoisha<br>10. Mwezeshaji atatilia mkazo vitu muhimu vilivyoandikwa kwenye chatipindu kutokana na majadiliano na kutoa ufafanuzi kama inawezekana<br>11. Mwezeshaji atoe hitimisho na kuwashukuru washiriki kwa usikivu wao</td></tr>
<tr><td>MAONI</td><td>Mwezeshaji anaweza kubadilisha maswali kadri itakavyombidi<br>Maswali yanayopendekezwa kwa ajili ya "Bakuli ya Samaki"<br>1. Unaelewa nini kuhusu MOTO?<br>2. Kwa nini uzuiaji na udhibiti wa moto ni muhimu kwako?<br>3. Utawezaje kujihusisha katika uzuiaji na udhibiti wa moto?<br>4. Tufanye nini ili kuboresha mafunzo haya</td></tr>
</table>

# Kiambatisho 1

## Vitini vya Masomo kwa Washiriki

Kumbuka: Vitini hivi viandaliwe kabla ya mafunzo na vigawiwe kwa washiriki

### Kitini Somo 1: Athari Chanya na Athari Hasi za Moto

Zipi ni athari hasi zinazoweza kutokana na moto?

- Kuchoma mazao, nyumba na mali hivyo huzidisha umaskini kwa kuharibu mali na fedha
- Kuharibu uoto wa asili kama vile misitu na mapori
- Kupoteza maisha ya viumbehai (binadamu, wanyama, mimea, wadudu na kadhalika)
- Uharibifu wa mazingira (vyanzo vya maji, udongo, viumbehai, ardhi, mabadiliko ya tabianchi na kadhalika)
- Kukua kwa chuki baina ya jamii
- Moshi husababisha ajali za barabarani




Kielelezo 1: Shamba lililoharibiwa na moto na maeneo ya jirani

## Zipi ni athari chanya zinazoweza kutokana na moto iwapo ukitumia kwa usahihi?

- Uondoaji wa nyasi zisizofaa na kuchochea ukuaji wa malisho bora
- Uondoaji wa uwingi wa Mwako/uoto ili kupunguza hatari ya moto wakati wa kilele cha msimu wa moto
- Njia ya kusafisha mashamba katika utayarishaji wa mashamba kwa ajili ya kupanda mazao




Kielelezo 2: Moto kwa ajili ya usimamizi wa malisho

## Kitini Somo 2: Pembetatu ya Moto

**Ili moto uwake ni lazima kuwe na vitu vitatu kwa pamoja.**

1. Oksijeni, ambayo ni gesi ya asili inayounda hewa na ipo juu ya hewa, uwingi wa oksijeni unaweza kuongezwa na kasi ya upepo

2. Halijoto (joto): Joto linaweza kuanzisha moto kutokana na kuwashwa kwa njiti, kutupa vijinga vya moto bila kuzimwa, moto kwa ajili ya utayarishaji wa mashamba, moto wa majumbani, kukausha samaki, urinaji wa asali na kuwinda wanyama.




Kielelezo 3: Pembetatu ya Moto

3. Vitu vinavyoungua (Mwako): Kuna aina tatu kuu za vitu vinavyoweza kuungua (i) vitu ambavyo si vizito na vinaweza kuvunjwa kwa mkono mmoja, huungua kwa haraka mfano nyasi kavu, majani na kadhalika (ii) vitu vya katikati ambavyo huvunjika kwa kutumia mikono miwili, haviwaki kwa urahisi ukilinganisha na vitu ambavyo si vizito kwa mfano miti midogo, matawi ya miti na kadhalika (iii) Vitu vizito ambavyo huchukua muda mpaka kuwaka moto na huungua taratibu mfano magogo, visiki na kadhalika

## Nini kifanyike ili kuzima moto?

- Ondoa kimojawapo katika vitu vitatu vilivyotajwa hapo juu kwa mfano ondoa oksijeni kwa kutumia matawi ya miti, mchanga, mifuko na kadhalika

## Utawezaje kuondoa vitu vilivyoungua?

- Ondoa kwa kuchimbua kinga-moto

## Utawezaje kuondoa Joto?

- Ondoa joto kwa kutumia maji au mchanga

## Mazingira ya Moto

- Kuwaka na kuenea kwa moto kunaweza kusababishwa na vigezo mbalimbali vya kimazingira kama vile hali ya hewa na umbile la ardhi..

## Hali ya Hewa:

- Upepo: Hubadilika na hauwezi kutabirika, upepo mkali huchochea mabadiliko ya ghafla ya uelekeo wa moto na hukuza kasi ya ueneaji wa moto, hivyo kufanya udhibiti wa moto kuwa mgumu.
- Kiwango cha unyevunyevu: Tabia za moto hutegemeana na uongezekaji au upunguaji wa unyevunyevu kwenye hewa, kwa mfano kama unyevunyevu ukipungua moto huongezeka.
- Halijoto: Ongezeko la joto huongeza ukaukaji wa vitu ambavyo huwaka na kukuza uwakaji wa moto na usambaaji wake. Kupungua kwa joto hupunguza matukio ya moto.

## Umbile la ardhi

- Miteremko: Katika mteremko mkali kasi ya moto huongezeka (iwapo moto ulianzia chini ya mteremko)
- Mlima: Moto katikati ya vilima viwili huwaka kwa kasi zaidi kutokana na kasi ya upepo. Moto utawaka zaidi kupanda mlima kuliko kushuka mlima
- Tambarare: Moto huwaka taratibu katika maeneo tambarare kama upepo hauna nguvu.

## Kitini Somo 3: Jamii na Matumizi ya Moto

Matumizi salama ya moto ni muhimu kwa ajili ya matumizi endelevu ya rasilimali, kutokana na ukweli kwamba jamii inatumia moto kwa madhumuni mbalimbali kama vile kilimo, maeneo ya malisho, moto unaodhibitiwa katika hifadhi za misitu, kuchoma takataka, ufugaji nyuki, moto katika kambi na kambi za uvuaji samaki, uzalishaji mkaa na kadhalika. Ili kufanikisha haya yote, jamii inalazimika kutumia moto katika njia salama bila kuleta madhara.

Hivyo, jamii inapaswa kufanya jitihada kubwa ya kuhakikisha kwamba maisha ya viumbe, misitu na mali inaendelea kuwepo na kusaidia jamii. Jamii inapaswa kufanya matumizi bora ya moto kama ifuatavyo:

### Ы Maandalizi ya mashamba na malisho ya mifugo

- Kuzingatia wakati na majira ya mwaka
- Kuomba ruhusa ya kuwasha moto kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji
- Kuweka kinga-moto au kutumia uzio
- Fahamisha jirani zako na wanakijiji wengine
- Kuwa na kikundi cha kuzima moto
- Kuandaa vifaa vya kuzima moto ili kuwa tayari iwapo moto utavuka mahali ulipowashwa
- Muda mzuri wa kuwasha moto ni jioni




Kielelezo 4: Moto usio na usimamizi

## Ы Ufugaji Nyuki

- Zingatia muda na msimu wa urinaji asali
- Omba ruhusa ya kurina asali kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji
- Weka kinga-moto au tumia uzio kuzunguka manzuki
- Usitumie moto kurina asali bali tumia bomba la moshi
- Andaa vifaa vya kuzima moto iwapo moto utawaka
- Urinaji uanze kabla ya saa nne asubuhi na baada ya saa saba mchana
- Zima moto pindi tu utakapowaka jirani na mizinga ya.

GIZ/ Unknown Source



Kielelezo 5: Kifaa cha kutoa moshi kwa ajili ya urinaji asali

### ЬЇ Msitu

- Zingatia muda wa uchomaji wa mapema na majira ya mwaka, mfano kwa kawaida ni kuanzia mwezi Aprili mpaka Julai.
- Omba ruhusa ya kuwasha moto kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji
- Weka kinga-moto au tumia uzio wa miti (live fence)
- Kuwa na kikundi cha kuzima moto
- Andaa vifaa vya kuzima moto iwapo moto utawaka
- Bainisha vyanzo vya maji yatakayotumika pindi moto utakapozidi



Kielelezo 6: Njia isiyo sahihi na njia sahihi ya kufukizia nyuki moshi wakati wa urinaji asali

- Ni vizuri zaidi kuwasha moto nyakati za jioni
- Fuatilia hali ya uwakaji wa mabaki ya moto kwa siku tatu

### Ӹ Uchomaji wa takataka

- Zingatia muda wa siku na majira ya mwaka
- Omba ruhusa ya kuwasha moto kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji
- Weka kinga-moto kuzuia kusambaa kwa moto
- Andaa kikundi cha kuzuia moto
- Hakikisha muda wote kuna mtu wa kuukagua moto
- Ni vizuri zaidi kuwasha moto jioni
- Fuatilia na zima mabaki ya moto yaliyobaki kwa siku mbili

### Ӹ Kutengeneza Mkaa

- Omba ruhusa ya kuchoma mkaa kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji
- Weka kinga-moto kuzuia kusambaa kwa moto
- Tumia teknolojia iliyoboreshwa ya uchomaji mkaa
- Afisa Mtendaji wa Kijiji awataarifu wanakikundi na wachoma mkaa ili wafuatilie hali jirani na tanuri la mkaa
- Andaa vifaa vya kuzimia moto pindi moto ukiponyoka (maji, majani, panga na kadhalika)
- Zima mabaki ya moto yaliyosalia wakati wa kufukua mkaa.



Kielelezo 8: Njia isiyo salama ya utengenezaji mkaa



Kielelezo 9: Njia salama ya kutengeneza mkaa

## Ы Maandalizi ya maeneo ya kuweka kambi na kuwasha moto

- Omba kibali cha kuweka kambi (kambi ya watalii, uvuvi, ukataji magogo na kadhalika) kutoka kwa ofisa aliyeidhinishwa kisheria
- Omba ruhusa ya kuwasha moto kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji
- Weka kinga-moto kuzuia kuenea kwa moto (kinga-moto kuzunguka mahali penye moto kwenye kambi, ondoa nyasi na kadhalika)
- Andaa vifaa vya kuzima moto iwapo moto utaenea (kwa mfano mchanga, maji)
- Zima mabaki ya moto wa kambi wakati mnaondoka kambini ama kwa maji au mchanga.




Kielelezo 10: Siku zote zima moto wako wa kambi au wa kupikia

# Kitini Somo 4 na 5: Ushiriki wa Jumuiya na Wajibu wao katika Usimamizi wa Moto

## Jumuiya ni wakina nani?

Jumuiya ni watu wote (watoto, vijana, watu wazima, wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara, wafugaji, wavuvi, viongozi wa dini, na kadhalika) ambao wanaishi katika eneo fulani na taasisi zote; (mashirika mbalimbali ya kidini, ofisi za serikali, taasisi za elimu, mashirika yasiyo ya kiserikali) ambayo yanatoa huduma mbalimbali katika eneo hilo. Watu hao hushiriki katika kuhakikisha kwamba maisha ya jamii na mali zao yako salama na kwamba mazingira yanalindwa..

## Ushiriki

Kila mwanajumuiya anatakiwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa moto kwa misingi ya sheria zinazohusiana na uhifadhi wa mazingira. Ushiriki wa jamii katika usimamizi wa moto unahitajika kutoka hatua ya awali hadi hatua ya mwisho ya utekelezaji. Kuwashirikisha wanajumuiya katika usimamizi wa moto ni mchakato ambao unahitaji utashi na utayari wa jamii ili;

- Kujenga uwezo wa jamii wa kuongoza mchakato
- Kuongeza uwazi kwa jamii.
- Kupunguza na kudhibiti migogoro ya kijamii juu ya rasilimali zilizopo.
- Kujenga uwezo wa jamii kwa ajili ya uendelevu Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii.

## Kujenga uwezo wa jamii

Kujenga uwezo wa jamii ni moja ya kanuni za msingi za usimamizi wa moto ambapo jamii inajenga ufahamu, kujiamini na stadi kwa njia ya mafunzo na kuhakikisha kuwa kamati ya mazingira, makundi ya watumiaji wa mazingira, viongozi wa vijiji na watu binafsi wanatumia mafunzo haya katika kutekeleza majukumu yao katika usimamizi wa moto.

## Kutosheleza mahitaji ya jumuiya

Wanajamii ambao wana haki ya umiliki wa kimila wa maeneo ya misitu kwa mfano kupitia Usimamizi Shirikishi wa Misitu au Usimamizi wa Pamoja wa Misitu wapewe nafasi ya kuhamasishwa ili waweze kutambua umuhimu wa usimamizi wa moto na faida wanazoweza kupata kutokana na shughuli hiyo.

## Uundaji wa vikundi vya usimamizi wa moto

Kujenga ushiriki wenye nguvu ni bora kwa jamii kuwa na kikundi kiongozi katika usimamizi wa moto katika ngazi ya kijiji. Kikundi hiki kitafanya kazi kwa ushirikiano na kamati za mazingira na jamii kwa ujumla. Idadi ya wajumbe wa kikundi cha usimamizi wa moto haipaswi kuwa zaidi ya kumi (10).

## Sifa ya wanachama wanaounda kikundi kiongozi katika usimamizi wa moto

- Kuwe na mchanganyiko wa wanaume na wanawake
- Kuwe na watu ambao ni wakareketwa wa uhifadhi wa misitu na mazingira
- Kuwe na mchanganyiko wa watu mbalimbali ambao hutumia moto katika shughuli zao, ikiwa ni pamoja na wakulima, wawindaji, wafugaji, wavunaji wa asali na watumiaji wengine wa moto
- Kuwe na wawakilishi kutoka kila kitongoji katika eneo husika.

## Majukumu ya kikundi kiongozi katika usimamizi wa moto

Kwa faida ya maisha ya watu, wanyama, wadudu, misitu na rasilimali nyingine ambazo zinawawezesha kukua na kuwa endelevu na kupunguza matishio ya moto kwa viumbe hai na rasilimali, lazima jamii iwajibike kudhibiti moto. Jamii na kikundi chake cha usimamizi wa moto inawajibika kuzuia na kudhibiti matishio ya moto kwa njia zifuatazo:-

1. Kupunguza matumizi ya moto wakati wa maandalizi ya mashamba, urinaji asali na uwindaji wanyama.
   a. Utoaji wa elimu juu ya matumizi bora ya moto kwa ajili ya usimamizi wa maliasili
   b. Ni lazima jamii itii sheria na sheria ndogo, pamoja na kufuata taratibu za matumizi bora ya moto.
   c. Kuimarisha maeneo ya usalama kwa ajili ya moto baina ya misitu au nyika na makazi
2. Kushiriki katika kuunda, kutekeleza na kusimamia mipango ya kazi.
3. Kuwa tayari kuzima moto pindi utakapotokea
4. Kuelimisha jamii juu ya matumizi na usimamizi wa shughuli zote za moto.
5. Kuandaa Mpango wa usimamizi wa MotoJamii kwa ajili ya eneo la jamii
   a. Kushirikisha jumuiya katika kubuni na kutekeleza mpango wa usimamizi wa MotoJamii
6. Kuratibu shughuli zote za moto ndani ya kijiji kulingana na sheria na kanuni za nchi.

7. Kutunza kumbukumbu za matukio ya moto na kuzisambaza kwa wadau wote wa moto.

8. Kuwasilisha taarifa mbalimbali zinazohusu jinsi ya kudhibiti moto katika mikutano ya kijiji.

9. Kutambua fursa zilizopo, changamoto na vyanzo vya moto usiodhibitiwa.

10. Kuwa tayari kushiriki katika kupambana na moto pindi unapotokea

11. Kutoa tahadhari ya moto kwa wadau, kwa wale wanaopita na wanakijiji wengine kwa mfano kuweka mabango.

12. Kusimamia sheria na kanuni za matumizi mazuri ya moto

## Kitini Somo 6: Tathmini ya Athari ya Moto

Maeneo ambayo jamii huishi yanaweza kuwa katika hatari iwapo hawatakuwa na vigezo ambavyo huwezesha usimamizi wa shughuli za moto kufanyika kwa urahisi na usalama.

Mambo yafuatayo huchangia sana kufanya maeneo ya makazi kuwa katika hatari zaidi:-

1. Kuwa na njia ndogo za usafiri za kuingia na kutoka (yaani 1), nyembamba (chini ya mita 6) na kuwa na barabara zenye hali mbaya wakati wote (haina lami au changarawe) na yenye mashimo makubwa.
2. Kutokuwa na huduma ya zimamoto na vigumu kwa gari kupita (gari haiwezi kugeuza)
3. Kutokuwa na ishara ya barabara au zipo lakini hazina mng'ao wa kutosha kutoa tahadhari kwa watumiaji.
4. Kuwa na uoto wa asili ambao umefungamana na rahisi kuungua
5. Kutokuwa na eneo la kujihami na moto (yaani mita 10 kutoka katika eneo fulani, kwa mfano msitu na makazi)
6. Kutokuwa na kizuizi cha moto
7. Kuwa na idadi kubwa ya miinuko ya asili
8. Kuwa na vyanzo vya moto kama vile; matukio ya radi mara kwa mara, umeme, utalii na kambi za kitalii
9. Kuwa na paa ambalo linashika moto kirahisi (mfano; nyasi)
10. Kuwa na vyanzo vichache vya maji / ukosefu wa maji (yaani ardhi kavu)
11. Upatikanaji mgumu wa huduma za mawasiliano (zaidi ya km 8 kutoka kwenye kituo)
12. Ukosefu wa vifaa vya kugundua moto yani mnara / kusini / mlima, simu ya mkononi, pamoja na kiashiria kwa ajili ya siku hatari ya moto)
13. Kutokuwa na wataalamu au watu wenye ujuzi na masuala ya moto (yaani, kikundi kiongozi)

### Ufahamu kuhusu usimamizi wa moto

Ni muhimu kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya usimamizi wa moto.

Pia ni vizuri kuijulisha jamii ukanda salama utakuwa wapi. Ukanda salama unaweza kuwa kiwanja cha soka au michezo, barabara au sehemu ya eneo ambalo limeshawaka moto. Pia ni vizuri kuijulisha jamii

kuhusu njia za mawasiliano ambazo zitatumika wakati wa msimu wa moto, mfano simu ya mkononi, kupiga tarumbeta, mabango ya moto na kadhalika. Ni vizuri kujua wapi ambapo vifaa vya kuzima moto vinapatikana au kuhifadhiwa. Vifaa vya kuzima moto ni kama, matawi ya miti, ndoo za maji au mchanga, majembe, makwanja, mapanga na kadhalika

Kwa ajili ya kuendelea kuwafikia wananchi, ni wajibu wa wadau mbalimbali kujenga uwezo wa kudhibiti moto, ni vizuri kwa wadau mbalimbali kuwa na sheria na kanuni za matumizi ya moto na mbinu za usimamizi wa moto.

## Wajibu wa wadau katika uzimaji moto

| Mdau | Wajibu |
|---|---|
| Wizara | Kuratibu Shughuli za moto na kutoa vifaa na wataalamu |
| Mkoa/Wilaya/Halmashauri | Kuratibu Shughuli za moto na kutoa vifaa na wataalamu |
| Hifadhi/Mashamba ya miti/Mazao/Malisho | Kuratibu Shughuli za moto na kutoa vifaa na wataalamu |
| Mashirika ya dini/elimu/siasa | Kutoa vifaa, wataalamu, sera na uhamasishaji |
| Jumuiya | Kushiriki katika kudhibiti moto |

Ni muhimu kufanya ukaguzi wa maeneo yenye hatari ya moto ili kujenga uwezo wa jamii kutathmini maeneo hatari ambayo ni vigumu kuyasimamia pindi moto ukizuka: ukaguzi unaweza kufanyika kwa kundi dogo na kutoa tathmini kwenye jamii nzima ili kurekebisha mapungufu yaliyofanya eneo husika kuwa eneo lenye hatari ya moto. Ni bora kuelimisha jamii jinsi ya kutumia fomu za ukaguzi wa eneo lenye hatari ya moto.

# Kitini: Mpango wa Usimamizi wa Moto katika Ngazi ya Jamii

Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii ni mpango kwa ajili ya kuzuia na kudhibiti moto wa kwenye misitu ambayo huathiri maisha ya watu na mali zao. Mpango huu unalenga kupunguza uharibifu unaosababishwa na kutokuwa makini kwenye jinsi ya kuzuia na kudhibiti moto. Mpango huu ni motisha kwa ajili ya usalama wa kiuchumi na hifadhi ya jamii katika kulinda maisha na mali. Faida ya Mmpango wa Usimamizi wa MotoJamii katika ngazi ya jamii ni kutoa nafasi ya kutosha kwa jamii katika kudhibiti moto na hatimaye kupunguza athari mbaya ya moto.

## Nani anawajibika kuandaa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii?

Ili kuwezesha shughuli za kuzuia na kudhibiti moto, jamii inahitajika kuandaa mpango wa utekelezaji ambao utatumika katika shughuli zao za kila siku. Mpango huu utaandaliwa kwa pamoja na kikundi cha MotoJamii pamoja na kikundi cha kuzima moto. Baada ya kikundi kiongozi kuandaa mpango wa utekelezaji, mpango utawasilishwa katika mkutano mkuu wa kijiji kwa kupitia kamati ya mazingira ili kukusanya michango zaidi na kupata idhini ya mwisho.

## Mambo ya kuzingatia wakati wa maandalizi ya Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii

Kabla ya kuandaa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii, ni muhimu kufanya tathmini ya athari za moto katika eneo fulani. Wakati wa tathmini ya moto mambo yafuatayo yanahitajika kutiliwa maanani;

1. Kubainisha maeneo yenye hatari ya moto: kutumia fomu ya ukaguzi wa maeneo yenye hatari ya moto; angalia somo la 7: Ukaguzi wa Maeneo yenye Hatari ya Moto
2. Vyanzo vya maji, ni muhimu kubainisha vyanzo vilivyopo vya maji na kama havipo ni hatua zipi zichukuliwe?
3. Vifaa vya moto, ni vyema kubainisha vifaa vya kuzimia moto ambayo vinapatikana ndani ya eneo hilo, pamoja na orodha ya vifaa ambavyo vimekosekana na ambavyo vinahitajika, pia kujua mahali ambapo vifaa vilivyopo vinahifadhiwa
4. Ni vizuri kujua njia inayotumiwa na jamii katika kutambua moto na maeneo ya kuangalia moto
5. Njia za kufikia jamii; nini kifanyike ili kuhakikisha kuwa maeneo hatarishi yanafikika kirahisi.
6. Wingi wa vitu vinavyoweza kuungua; Ni bora kujua njia ambazo zitatumika kupunguza vitu vinavyoweza kushika moto katika eneo husika
7. Kujenga uelewa juu ya udhibiti wa moto

Ni muhimu kuwa na ushirikiano katika usimamizi wa moto ndani ya jamii ili kuipa changamoto jamii katika suala la kudhibiti moto. Na ni bora kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kikundi kiongozi cha kudhibiti moto. Ni muhimu pia kwa jamii kujua sehemu ambapo mafunzo hutolewa.

## Mfano wa Muundo wa Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii katika Kijiji

1. Utangulizi.
2. Taarifa za Kijiji.
3. Lengo la mpango.
4. Wadau wa usimamizi wa moto katika jamii na majukumu yao
5. Muda wa mpango.
6. Tathmini ya athari za moto.
7. Jukumu na kazi za wadau mbalimbali katika kuzuia na kudhibiti moto.
8. Uelewa juu ya njia za kuzuia na kudhibiti moto.
9. Ufuatiliaji na tathmini.
10. Viambatisho

# Kiambatisho 2

## Fomu ya Ukaguzi wa Hatari ya Moto

Mwezeshaji aelezee jinsi ya kutumia fomu hii

| Vigezo | Alama (Halisi) | Alama (Iliyorekebishwa) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| Njia ya usafiri katika eneo husika | | | |
| Njia za kuingia na kutoka katika ukanda wenye hatari ya moto | | | |
| Barabara 1 au 2 nje au ndani ya eneo husika | 0 | | |
| Njia ya kuingia na kutoka katika eneo lenye hatari ya moto | 7 | | |
| Upana wa barabara | | | |
| ≥ 6 mita | 0 | | |
| ≥ 6 m na < 7 mita | 2 | | |
| < 6 mita | 4 | | |
| Hali ya barabara katika mwaka | | | |
| < 5% mashimo | 0 | | |
| > 5% mashimo | 2 | | |
| < 5% mawe/changarawe | 2 | | |
| > 5% mawe/changarawe | 5 | | |
| Huduma za zimamoto za manispaa na ufikaji wa barabara | | | |
| ≤ 90m kwa gari kurudi nyuma | 0 | | |
| > 90m kwa gari kurudi nyuma | 2 | | |
| < 90m bila kurudi nyuma | 4 | | |
| ≥ 90m bila kurudi nyuma | 5 | | |
| Alama za barabarani | | | |
| 15c zinazoakisi mwanga/zinazong'ara | 0 | | |
| Hazipo | 5 | | |
| Uoto wa asili | | | |
| Uoto uliotapakaa kila mahali/jirani ya makazi | | | |
| Kidogo (Kidogo/ wastani/mwingi) | 5 | | |
| Wastani (aina fupi ya nyika , misonobari) | 10 | | |
| Mwingi (miti iliyokaribiana inayovamia) | 20 | | |
| Eneo la kujikinga na moto | | | |

| Vigezo | Alama (Halisi) | Alama (Iliyorekebishwa) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| Mita 30 za kuweka uoto mbali na makazi | 1 | | |
| 21 – 30/ za kuweka uoto mbali na makazi | 3 | | |
| 11-20m za kuweka uoto mbali na makazi | 10 | | |
| 10m za kuweka uoto mbali na makazi | 25 | | |
| Barabara ya kupambana na moto | | | |
| Inatosha | 0 | | |
| Haitoshi | 10 | | |
| Hakuna | 25 | | |
| Hali ya miinuko ya asili iliyoshamiri 91.4m | | | |
| Miteremko > 9 % | 1 | | |
| Miteremko 10% mpaka 20% | 4 | | |
| Miteremko 21 mpaka 30% | 7 | | |
| Miteremko 31% mpaka 40% | 8 | | |
| Miteremko > 41% | | | |
| Vipimo zaidi | 0-5 | | |
| Ugawanywaji wa miinuko ya asili na madhara yake (Makorongo na miinuko ya wastani) | | | |
| Vyanzo vya hatari ya moto | | | |
| Matukio ya radi mara kwa mara | 0-5 | | |
| Reli | 0-5 | | |
| Milima | 0-5 | | |
| Umeme | 0-5 | | |
| Utalii na kambi za utalii | 0-5 | | |
| Maeneo yenye hatari ya moto | 0-5 | | |
| Uwepo wa matukio ya moto | | | |
| <Km1 mpaka km 1 ya mraba | 1 | | |
| 2 - 4 mpaka km 2 za mraba | 2 | | |
| Km 5-7 za mraba | 3 | | |
| km Km 7 -10 za mraba | 5 | | |
| > km 10 za mraba | 10 | | |
| Vitu vinavyotumika zaidi kukwangulia nyumba | | | |
| Vitu vya kawaida | | | |

| Vigezo | Alama (Halisi) | Alama (Iliyorekebishwa) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| Paa lisiloshika moto (mabati) | 0 | | |
| Paa linaloungua taratibu (vigae) | 5 | | |
| Paa linaloungua haraka (Nyasi) | 25 | | |
| Matatizo ya ujenzi wa nyumba kwenye miteremko 30% au zaidi | | | |
| Mteremko wa ≥ 10m | 1 | | |
| Mteremko wa <10m | 5 | | |
| Udhibiti wa moto uliopo | | | |
| Vyanzo vya maji katika eneo husika | | | |
| Vyanzo vya maji lita za ujazo ~ 2000 | 0 | | |
| Vyanzo vya maji lita za ujazo ~1000 | 5 | | |
| | 10 | | |
| Kuna upungufu wa maji | | | |
| Upatikanaji wa vituo vya mawasiliano | 1 | | |
| ≤ 8km kutoka kwenye kituo | 3 | | |
| > 8km kutoka kwenye kituo | | | |
| Vifaa vya ugunduzi wa moto | 1 | | |
| Mnara/ Kichuguu/ Mlima | 2 | | |
| Simu ya mkononi | 4 | | |
| Viashiria vya siku ya hatari ya moto (bendera nyekundu) | 6 | | |
| Taarifa za satelaiti | 10 | | |
| Hakuna | | | |
| Uanachama wa chama cha udhibiti wa moto | 0 | | |
| Ndio | 20 | | |
| Hapana | | | |
| JUMLA | | | |

## Tathmini ya maafa

| Maelezo | Jumla ya Alama |
|---|---|
| Kidogo | <40 |
| Wastani | 40 - 64 |
| Maafa makubwa | 65 - 109 |
| Maafa makubwa zaidi | >109 |

# Kiambatisho 3

## Nyenzo za Uwezeshaji

### Njia za Kutengeneza Makundi

Kuna njia mbalimbali za kutengeneza makundi; baadhi yake ni kama ifuatavyo:

- Mwezeshaji awaweke pamoja washiriki ambao hawafahamiani
- Mwezeshaji awaombe washiriki waunde makundi na watu wasiofahamiana nao kwa lengo la kubadilishana ujuzi. Idadi ya makundi itategemeana na mahitaji
- Boti inayozama: Mwezeshaji awaambie washiriki kuwa wao ni abiria katika meli ya Titanic. Waunde makundi kwa haraka kutokana na idadi ya watu watakaotajwa. Sema "Meli inazama tengeneza kundi la watu 6"
- Makundi ya sifa moja: Haya ni makundi ya watu wenye shauku au ufahamu wa aina moja. Kwa mfano wale ambao wana shauku na masuala ya kilimo na wanyamapori.
- Vitu vya aina moja: Angalia vitu vinavyoonekana na washiriki ambavyo vitaweza kukusaidia kutengeneza makundi kwa mfano viatu vyeusi au vya kahawia na rangi nyingine, fulana, mashati, blauzi, wenye miwani au wasio na miwani

## Vivunja Ukimya

### Mchezo wa wanyama

Mwezeshaji atengeneze vipande vya karatasi kwa kila mshiriki katika kundi kubwa. Mwezeshaji aandike jina la mnyama katika kila kipande cha karatasi, na atumie wanyama tofauti kwa makundi madogo yanayohitajika. Mwezeshaji awape washirki hivi vipande vya karatasi bila kujali mtiririko na awaambie wataje kwa sauti jina la mnyama ambalo kila mmoja amepewa ili wengine wenye jina kama hilo wasogee na kutengeneza kundi.

### Matunda mchanganyiko

Mwezeshaji awagawe washiriki katika makundi ya watu 3 au 4 ya mfano wa matunda kama vile chungwa, ndizi, embe. Ikifuatiwa na washiriki kukaa kwenye viti (bila meza) katika mduara na mshiriki

mmoja anapaswa kukaa katikati ndani ya mduara. Mwezeshaji ataje kwa sauti kubwa jina la tunda kwa mfano Chungwa! Wale walio katika kundi machungwa wanapaswa kubadilishana nafasi zao za kukaa (bila ya kusogeza viti) mshiriki moja karibu na katikati ya mduara atatakiwa kuchukua nafasi moja kati ya viti ambapo mshiriki mmoja atabaki bila ya kiti katikati ya mduara. Mshiriki ambaye alibakia bila kiti atataja kwa sauti jina la tunda jingine na mchezo utaendelea hivyo. Wakati matunda mchanganyiko yanatajwa, ina maana kuwa washiriki wote watabadilishana viti vyao.

## Usijibu.

Washiriki wasimame katika mduara, mtu mmoja aende kuelekea kwa mshiriki mwingine na kuuliza swali rahisi kwa mfano ni kitu gani kinakutia kinyaa zaidi? Mshiriki ambaye ameulizwa swali hapaswi kujibu, lakini mtu aliye upande wake wa kushoto anapaswa kujibu. Majibu si lazima yawe ya kweli, yanaweza kuwa ya rika/umri mmoja. Mchezo utaendelea kwa namna hiyo wakati yule anayeuliza maswali anaendelea kuwauliza washiriki tofauti.

## "Prrr" na "Pukutu"

Mwezeshaji awaongoze washiriki kuigiza kama ndege mmojawapo kati ya ndege hao wawili. Upande mmoja anapaswa kuitwa 'prrr' na upande mwingine uitwe 'pukutu'. Watu walio katika upande mmoja wote wasimamie vidole yao vya miguu na kutanua mikono yao wakati imekunjwa kama mabawa ya ndege. Iwapo ukiita 'pukutu', kila mtu katika kikundi lazima asimame kimya bila kugusa manyoya yake.

## Kuna mabadiliko yoyote?

Washiriki wajigawe katika jozi. Kila mtu amwangalie mwenzake na akariri muonekano wake. Kisha mmoja wao ageuke nyuma na kufanya mabadiliko katika muonekano wake kwa mfano avae saa katika mkono tofauti na wa mwanzo, kuvua miwani na kukunja mikono ya shati.

Mshiriki mwingine ageuke na kujaribu kubainisha mabadiliko yaliyofanywa na mwenza wake, washiriki wabadilishane na kufanya kama mwanzo.

# Kiambatisho 4

## Mfano wa Mada ya Mafunzo

### Malengo ya Mafunzo

- Ifikapo mwisho wa mafunzo washiriki wataelewa athari hasi na athari chanya za moto na matumizi salama ya moto kwa madhumuni mbalimbali ya maisha.
- Ifikapo mwisho wa mafunzo washiriki wataweza kuelewa majukumu na wajibu wa jamii katika kuzuia na kudhibiti moto.

### Siku 1

| Muda | Mada | Malengo | Shughuli |
|---|---|---|---|
| 02:30<br>03:30<br>04:00 | Ufunguzi wa mafunzo<br>Utangulizi wa mafunzo | Ifikapo mwisho wa somo: washiriki wataweza kufahamiana na kukubaliana sheria na kanuni za mafunzo | Uwasilishaji mada<br>Kadi za manila<br>Majadiliano ya kundi lote |
| 04:30 - 06:30 | Mapumziko ya Chai | Ifikapo mwisho wa somo; washiriki wataweza kuelezea athari za moto katika misitu na mali za jumuiya | Majadiliano katika vikundi vidogo |
| 04:30 - 06:30 | Athari chanya na athari hasi za moto | Ifikapo mwisho wa somo; washiriki wataweza kuelezea athari za moto katika misitu na mali za jumuiya | |
| 06:30 - 08:00 | Chakula cha mchana | | |
| 08:00 - 09:30 | Pembetatu ya moto | Ifikapo mwisho wa somo; washiriki wataweza kuelezea maana ya moto na vitu vitatu vinavyohitajika kuufanya moto uendelee kuwaka na namna ya kuzima moto kwa kuondoa kitu kimoja katika vitatu hivyo | Majadiliano ya vikundi vidogo |
| 09:30 - 10:00 | Mapumziko ya Chai | | |
| 10:00 - 10:30 | Maoni | Ifikapo mwisho wa kipindi mwezeshaji ataweza kuelewa hisia za washiriki juu ya somo lililofundishwa. Mwezeshaji ataweza kujua kiwango ambacho washiriki wameelewa masomo yaliyopita | Kipimo cha hisia |

## Siku 2

| Muda | Mada | Malengo | Shughuli |
|---|---|---|---|
| 02:00 -04:00 | Kupitia Siku 1<br>Jumuiya na matumizi ya moto | Ifikapo mwisho wa somo; washiriki wataweza kuelezea matumizi sahihi ya moto | Kadi za manila<br>Kazi za vikundi vidogo<br>Majadiliano ya kundi lote |
| 04:00 -04:30 | Mapumziko ya chai | | |
| 04:30 - 06:30 | Ushiriki wa jumuiya katika usimamizi wa moto | Ifikapo mwisho wa somo; washiriki wataweza kuelezea maana ya jumuiya na ushiriki wa jumuiya katika usimamizi wa moto | Kazi ya kikundi |
| 06:30-08:00 | Chakula cha mchana | | |
| 08:00-10:30 | Wajibu wa jumuiya katika usimamizi wa moto | Ifikapo mwisho wa somo; washiriki wataweza kubainisha wajibu wa jumuiya katika usimamizi wa moto | Uwasilishaji mada<br>Kadi za manila<br>Majadiliano ya kundi lote |
| 16:30-17:00<br>10:30-11:00 | Kufunga siku 2 | | |

## Siku 3

| Muda | Mada | Malengo | Shughuli |
|---|---|---|---|
| 02:00 - 04:00 | Kupitia siku 2<br>Uandaaji wa mpango wa usimamizi wa MotoJamii | Ifikapo mwisho wa somo;<br>Washiriki wataweza kuelewa umuhimu wa mpango wa usimamizi wa MotoJamii | Kadi za manila<br>Kazi za vikundi vidogo<br>Majadiliano ya kundi lote |
| 04:00 - 04:30 | Mapumziko ya Chai | | |
| 04:30 - 06:30 | Kubainisha maeneo yenye hatari ya moto (zoezi la nje) | Ifikapo mwisho wa somo; washiriki wataweza kutambua maeneo yenye hatari ya moto katika kijiji | Kazi ya kundi |
| 06:30 - 08:00 | Chakula cha mchana | | |
| 08:00 -10:00 | Endelea na mazoezi katika eneo la mafunzo na kumalizia Mpango wa Usimamizi wa MotoJamii | Ifikapo mwisho wa somo; washiriki wataweza kutambua maeneo yenye hatari ya moto katika kijiji | Uwasilishaji mada<br>Kadi za manila<br>Majadiliano ya kundi lote |
| 10:30 - 11:00 | Tathmini na Hitimisho | | Uwasilishaji mada |

# Kiambatisho 5
## Tathmini ya Mafunzo

1. Mafunzo uliyoyapata yana umuhimu gani?
2. Ni mada ipi imekuvutia sana?
3. Mafunzo uliyoyapata yatakusaidia vipi katika kudhibiti moto?
4. Kuna kitu chochote ungependa kujifunza juu ya moto?
5. Una mawazo gani juu ya ubora wa mwongozo wa mafunzo uliotumika katika mafunzo haya?
6. Unatoa mwongozo mzuri katika kufikia malengo ya mafunzo
7. Taarifa zinazotolewa ni za muhimu?
8. Nini kiboreshwe katika mwongozo huu?
9. Unashauri nini kuhusu mbinu zilizotumika kufikisha ujumbe?
10. Mbinu ipi ni ya muhimu, na ipi siyo? Toa maoni yako juu ya kuboresha mbinu hizo
11. Toa maoni yako juu ya kuboresha mafunzo;
12. Usafiri
13. Chakula
14. Umuhimu wa kutumia siku mbili kwa mafunzo haya
15. Unasemaje kuhusu kujifunza zaidi juu ya masuala ya moto?
16. Je mafunzo uliyopata yamekidhi haja zako?
17. Taja udhaifu wa mafunzo uliyopata




Tanzania Forest Services Agency
P. O. Box 40832 Dar es salaam
Email: mpingo@tfs.go.tz